

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUHIGWE
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu/ Fax 255 028 2810 339
Email: buhigwede2013@gmail.com



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P 443
BUHIGWE

Kumb Na BHDC/C.4/10/68

TAREHE 27/03/2018

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI.

1. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe anapenda kuwatangazia Wananchi wote wa Tanzania wenye sifa za kuajiriwa katika Utumishi wa umma kuomba kazi kwa nafasi ya **MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe.**

1.0 MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III (NAFASI 23)
(A) SIFA ZA MWOMBAJI:

- I. Awe na cheti cha kuhitimu na kufaulu kidato cha Nne (IV) au cha Sita (VI)
- II. Aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika fani ya Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma, au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
- III. Awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwadilifu mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 45.

(B) KAZI/MAJUKUMU:

- I. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- II. Kuwa mlinzi wa Amani na Usimamizi wa utawala Bora katika Kijiji
- III. Kuratibu na Kusimamia upangaji na Utekelezaji wa Mipamgo ya Maeneleo ya kijiji
- IV. Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- V. Kutafsiri na Kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- VI. Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Kazi ktika eneo lake na khamsisha wananchi katika kuandaa na utekelezaji wa mkakati kuondoa umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- VII. Kusimamia, Kukusanya na Kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.
- VIII. Mwenyekiti wa kikao cha wataalamu waliopo kwenye Kijiji
- IX. Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji
- X. Kupokea, kusikiliza na Kutatua Malalamiko na Migogoro ya wananchi

(C) MSHAHARA: Atalipwa Mshahara katika ngazi ya TGS B.

1.1. JINSI YA KUTUMA MAOMBI:

Barua zote ziandikwe kwa Mkono wa mwombaji na kutumwa kwa njia ya Posta kwa Anuani ifuatayo:

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe,
S.I.P 443
BUHIGWE/KASULU.

1.2. MUHIMU:

- a) Barua zote zitumwe kuitia posta , Barua zitakazoletwa kwa Mkono hazitapokelewa.
- b) Barua, anuani anayotumia kwa sasa pamoja na namba za simu zikiambatishwa na:
 - Maelezo Binafsi(CV)
 - Nakala ya Vyeti vya taaluma,
 - Nakala ya Cheti cha Kuzaliwa
 - Picha 2 za passport Size za hivi karibuni
- c) Awe hajawahi patikana na kosa lolote la Jinai
- d) Testimonials na Provisional Results havitakubalika
- e) Nakala zote za vyeti zithibitishwe na Hakimu au wakili Yeyote aliyesajiliwa na kuthibitishwa.
- f) Watakaochaguliwa kuhudhuria usaili (Short-listed) watafahamishwa kuitia anuani na namba za simu walizoaandika kwenye barua zao za maombi ya kazi.

1.3 NB: Mwisho wa kupokea Maombi haya ni Tarehe 10/04/2018 siku ya Jumanne saa 9:30 Alasiri

Pia tangazo hili waweza kulipata kuitia Tovuti yetu www.buhigwec.go.tz
Imetolewa na



Anosta L. Nyamoga
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUHIGWE

*MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
BUHIGWE*

NAKALA:

- I. Jalada:BHDC/C.4/10.68
- II. Mbao zote za Matangazo